Somo la 19.

Somo la 19 MAFUNZO YA BIBLIA KUHUSU IBILISI (Sehemu ya 2)

"Malaika wa Bwana akajiweka njiani kama shetani juu ya Balaamu" Hesabu 22:22.

"Yesu akamwambia Petro, Nenda nyuma yangu, Shetani; maana huyawazi yaliyo ya Mungu, bali ya wanadamu" Mathayo 16:23.

'SHETANI' ni neno la kawaida la Kiebrania linalomaanisha 'Adui' na hivyo hutafsiriwa kwa zaidi sana kwa matukio ya Agano la Kale. Katika baadhi ya sehemu, watafsiri, kwa sababu fulani, wanachagua kuhamisha neno kiholela badala ya kuitafsiri vizuri. Kama wangekuwa na uthabiti, matokeo yangekuwa ya kuvunjilia mbali nadharia ya ' Ibilisi jitu.'

Ni jambo la manufaa kujifunza matukio yote ya neno 'Shetani' katika Agano la Kale. Kuna mengi ya kujifunza kutokana na kupitia kwa makini vifungu hivi. Itabainishwa, katika kila hali ila moja (1 Mambo ya Nyakati 21:1) kwamba wakati ambapo linatafsiriwa 'Shetani' pembezoni daima inaonyesha 'adui' (pembezoni hutokea tu mwanzo kwa ajili ya kurejelea shetani wa Ayubu, lakini inatumika kila mahali). Kama vifungu vinachunguzwa kwa haki na uaminifu, kuunga mkono kokote dhahiri kwa nadharia ya Ibilisi jitu wa jadi kulingana na neno 'Shetani' kunatoweka kabisa. Kumbuka kwamba katika (Hesabu 22: 22,32) malaika wa Mungu anaitwa 'shetani'; pia katika 1 Samueli 29: 4 kumbuka kuwa Wafilisti walimchukulia Daudi kuwa 'shetani' kwao. Daudi alizungumza kuhusu wapwaa wake mwenyewe (wana wa Seruya) kama 'mashetani' (2 Samuel 19:22). Mara mbili Mungu aliwainua 'mashetani' binadamu kumwadhibu Sulemani (1 Wafalme 11:14, 23, 25) Hata hivyo hapo nyuma, wakati alipokuwa mtiifu, hakukuwa na 'mashetani' wa kumsumbua (1 Wafalme 4: 5).

MUNGU ANAITWA 'SHETANI' KWA ISRAELI WAOVU Katika mfano mojawapo Mungu mwenyewe alijulikana kama 'shetani' (adui) kwa Israeli kwa sababu ya uasi wao kwake. Kama malaika wa Mungu anaweza kuwa shetani (adui) kwa mtu mbaya (Balaamu), basi ni sahihi kabisa kwa Mungu mwenyewe kuwa shetani (adui) kwa watu waovu. Linganisha akaunti mbili zilizo sambamba ya tukio moja –

"Hasira ya Bwana ikawaka juu ya Israeli, naye (Bwana) akamtia Daudi nia juu yao, akisema, Nenda, ukawahesabu Israeli na Yuda ..." (2 Samweli 24: 1)

"Shetani akasimama juu ya Israeli, akamshawishi Daudi kuwahesabu Israeli" (1 Mambo ya Nyakati 21: 1)

Mungu hasababishi watu kutenda dhambi. Tabia za kupenda dhambi zinazotokana na maumbile asili ya binadamu tunayorithi hutufanya kutenda maovu ambayo matokeo yake ni mabaya sana, sio tu kwa mhusika, lakini pia huwa na ushawishi mkubwa kwa wote wanaomzunguka. Daudi alitambua makosa yake mwenyewe, na aliadhibiwa kwa kitendo hicho. Mungu daima ni mwenye haki na hana dosari, lakini ana haki kamili - kama Muumba wa vyote - kutekeleza sheria zake na

kuwaadhibu watenda dhambi kwa namna yoyote atakavyo. Ikiwa tutayakaribisha mawazo ya dhambi kimakusudi, Mungu anaweza kupanga kwamba tuongozwe ili tukose na makossa hayo yaanikwe wazi na kuadhibiwa, kwa kuwa mawazo ya dhambi yenyewe ni dhambi, na yanafaa kuadhibiwa (Mathayo 5:28). Mungu huadhibu kwa wema na upendo, ili apate kuturekebisha kwa kutuokoa kutoka katika dhambi mbaya zaidi, na kukataliwa mwishowe.

Kwa nini, walipojua ‘adui’ ni nani kutoka katika kifungu kinachoenda sambamba na kingine Watafsiri wa AV (toleo la mwanzo la Kiingereza na Kiswahili) walitumia 'Shetani' hapa, badala ya kutafsiri vizuri, kama mahali pengine ambapo wao hawakuwa na la kufanya, ambapo neno 'Shetani' lingepotosha maana?

Itafaa ieleweke kwamba katika Zaburi 109:6 na Zekaria 3:1-2, ambapo wana 'Shetani' katika maandishi, wana 'adui' pembezoni, kutupilia mbali kabisa nadharia ya Ibilisi jitu. Kwa kweli, katika sehemu zingine tatu katika Zaburi hiyo, neno hilo limetolewa kwa usahihi kama 'adui' Na hata katika mstari wa 6 ambapo wana 'Shetani. Kanuni kuu ya usambamba katika mashairi ya Kiebrania - (kusema kitu kimoja mara mbili kwa maneno tofauti: tazama Zaburi 105 yote kwa mfano wa kujitokeza wazi) - unathibitisha maana ya kweli –

"Weka mtu mbaya juu yake, na mruhusu Shetani (adui) asimame kwenye mkono wake wa kulia."

'SHETANI' WA ZEKARIA 3:1,2

'Shetani' wa Zekaria 3:1-2 ambaye anampinga Yoshua katika maono ya ishara iliyo wazi kwa mfano wa maandishi ya kihistoria ya kipindi hicho

"Ndipo akasimama Yoshua…wakaijenga madhabahu...maana hofu imewashika kwa sababu ya watu wa nchi hizo. Basi adui wa Yuda na Benyamini waliposikia ya kuwa wanamjengea BWANA hekalu…basi wakaja . . kisha watu wa nchi wakawafanya wawe dhaifu, na kuwasumbua, na Wakawaajiri washauri juu yao ili kupinga kusudi lao na kuandika mashtaka dhidi yao.. (Ezra 3: 2-3; 4: 1)

Hapa ni mfano ulio wazi katika maandiko matakatifu kuhusu ushetani. Mshitaki 'ni mojawapo ya maana za Kiyahudi ya neno 'shetani'.

'SHETANI' WA AYUBU

Hii inatuachia tu rekodi ya Ayubu ambapo neno 'Shetani' hutokea (lakini huko tena, katika AV ya Kiingereza, inafichua neno 'adui' pembezoni)…kuanzishwa kwa nadharia ya Ibilisi jitu katika Ayubu ni kitu kisichokubalika kabisa. Huyu 'Shetani' au 'adui' ni ‘miongoni mwa wana wa Mungu' (waabudu) waliokuja 'kujihudhurisha mbele za Bwana' (Ayubu 1:6). Kupata taswira ya Ibilisi wa jadi katika hali hiyo inaleta mkanganyiko, na inasaliti kanuni ya chini sana ya Mungu. Kuona hii kwa jinsi inavyofaa kuonekana - adui wa Ayubu, mcha Mungu ambaye alikuwa na wivu na kijicho na Ayubu kwa vile Mungu alikuwa amempata neema - ni jambo la

kawaida kwa mwanadamu, na ni picha ambayo mtu yeyote angeipata kama ingetafsiriwa kwa usahihi. Kusema kuwa Mungu angejadili na kubishana na jitu linalokaribiana naye kwa nguvu - kama theolojia ya jadi inavyotaka tufikirie - na kumpa uwezo wa kumleta mtumishi mwaminifu wa Mungu Ayubu kwenye mlango wa mauti, inaelezea kina cha machafuko ambamo dini pendwa imezama.

Aliyeleta maafa yote juu ya Ayubu, maelezo yakisomwa kwa makini yataonyesha kuwa nguvu hizo zinazozidi za wanadamu zilizodhihirishwa zilikuwa za Mungu, na kuthibitiwa na Mungu - "Ujapokuwa ulinichochea (Mimi Mungu) dhidi yake (Ayubu).ili nimwangamize "(Ayubu 2: 3). "Mkono wa Mungu umenigusa" (Ayubu akizungumza) - Ayubu 19:21.

"Basi ndugu zake wakamtuza moyo wake katika habari za huo uovu wote Bwana aliouleta juu yake" (Ayubu 42:11).

Hii kauli ya mwisho ni ya msimulizi aliyeongozwa na pumzi ya Mungu, na anathibitisha maneno ya Ayubu mwenyewe. Kweli, inasema kwamba –

"Basi Shetani akatoka… akampiga Ayubu na majipu mabaya.." (Ayubu 2: 7) vifungu vingine vya juu vinaonyesha wazi kwamba nguvu hii ni ya Mungu. Huwa mara nyingi tunawapata watu wa kawaida wakiwa na uwezo wa kutenda mambo yasiyo ya kawaida, kama inatekeleza madhumuni ya Mungu. Nasi tunaona hali kama hii ikisemwa kana kwamba wote wawili, Mungu akitenda yaliyotukia, na vilevile binadamu akitumiwa kama wakala kutenda yayo hayo.

Akizungumzia mapigo ya Misri (ambayo ni pamoja na mateso ya majipu), tunaambiwa:

"Bwana akasema na Musa, Mwambie Haruni, Nyosha mkono wako na usababishe vyura waje". . .

"Musa na Haruni wakafanya maajabu hayo yote: (Kutoka 8: 5; 11:10)

Na hata katika muktadha sawa (kama hapa kwa Ayubu), inaelezwa kuwa Mungu ndiye mtendaji.

ADUI MKUBWA WA MWANADAMU NI DHAMBI

Adui mkubwa wa wanadamu wote ni Dhambi katika mwili; maovu, 'mwenendo wa dhambi' wenye uasi ndani ya miili yote ya wanadamu; 'Fikira za kimwili' ambayo, Paulo anasema, ni –

"Nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kutii "(Warumi 8: 7).

Hii kanuni mbaya iliyo hali ya binadamu iliyoota mizizi zilimfanya Paulo kuongezea zaidi kusema ...

" Mimi ni mtu wa asili ya kimwili, kuuzwa chini ya Dhambi. . Dhambi ndani yangu ... Katika mwili wangu halikai neno jema… Dhambi inaishi ndani yangu ... Naona sheria katika viungo

vyangu. . sheria ya Dhambi katika viungo vyangu ... Watu waliopo kwenye mwili hawawezi kumpendeza Mungu. . Kama mkiishi kwa mwili mtakufa. . sababu mwili hutamani ukishindana na Roho "(Warumi 7: 14,23; 8: 8; Wagalatia 5:17).

Hii inaweza kuongezwa mara nyingi, kuonyesha Shetani wa Biblia. Baadhi ni hizi ...

" Kwa maana moyoni hutoka mawazo mabaya,uuaji, uzinzi,uasherati wizi, nk "(Mathayo 15:19).

" Basi matendo ya mwili ni: uzinzi, chuki, hasira,uasherati, uadui, ugomvi,fitina,uuaji nk ". (Wagalatia 5:19 21)"

YOTE yakiopo katika ulimwengu - tamaa ya mwili, tamaa ya macho na majivuno ya maisha – sio ya Baba, bali ni ya ulimwengu "(I Yohana 2:16)

Kwa hiyo tunaona katika Agano Jipya, neno 'Shetani, au' adui, linatumika kwa kanuni hii ya uovu katika mwili wa binadamu, katika sura yake mbalimbali, kibinafsi na kisiasa.

Neno 'shetani' lilibebwa kutoka katika lugha ya Kiebrania hadi kwa Kigiriki ya Agano Jipya. Wacha tukadirie matukio ya neno 'shetani' katika Agano Jipya ... Kama vifungu hivi vitachunguzwa, vyote vitaonekana kuingiana ndani ya muundo wa kanuni wa neno hili kuwa dhambi, au kwa mtu binafsi au mikusanyiko inayoendeshwa au kupewa motisha na kanuni hizo (isipokuwa katika mfano mmoja ambapo Kristo, akizungumza na Mafarisayo 'kwa mafumbo’ (Marko 3:22 26 Mathayo 12: 24,27), anayachukua majina yao ya kishirikina - Beelzebuli, Shetani - na kuwachanganya nayo.

PETRO ALIKUWA 'SHETANI'

Petro, katika upendo, akipotoshwa na mvuto wa mwili (Shetani), alipingana na Kristo juu ya kifo chake kama sadaka. Yesu alisema - "Nenda nyuma yangu Shetani! Unayawazia mambo ya watu" (Mathayo 16:23, Marko 8:33).

Petro alipewa motisha na hisia za kimwili, na kwa upofu wa kimaumbile uliokuwa kinyume na nia na madhumuni ya Mungu na kinyume na hekima ya kweli na wema. Kwa hakika hakukuwa na nguvu zisizo za kawaida za kiibilisi zilizohusika. Kumwita 'shetani' katika maana ya maandiko matakatifu ilifaa kabisa, na ingawa alikuwa na nia 'nzuri, alipotoka. Lakini kumwita 'Shetani' chini ya hali hii kama ilikuwa ni ishara mbaya, kiothodoksi, Mungu anavyochukia Ibilisi, ingekuwa ni jambo gumu kwa Kristo kumkemea kwa upendo wake potofu wa kimwili kwa Bwana wake. Petro hakika alikuwa 'adui' kwa lengo la Mungu katika pingamizi lake la kifo cha Kristo kama dhabihu, lakini mtazamo maarufu wa jadi, inatuhitaji kuamini kwamba Kristo alimtambulisha Petro na jitu ambalo ni mfano kabisa wa kiumbe halisi na mkubwa aliyekithiri kina cha uzembe na maovu.

Kuna mfano kama huo wa maelezo kuhusu kuonyesha 'Shetani' wa Biblia ni nini hasa katika Matendo 5. Peter alisema:

"Anania, kwa nini Shetani ameujaza moyo wako kumwambia uongo Roho Takatifu" (kifungu cha 3).

Kisha kuonyesha kitu kile kwa maelezo wazi, alisema (k.4)

"Kwa nini basi, uliamua jambo hili moyoni mwako?"

Na baadaye kidogo kwa mkewe Anania, Safira, alisema (k. 9)

"Kwa nini ninyi mmekula njama kumjaribu Roho wa Bwana?"

PAULO 'MJUMBE WA SHETANI'

Usambamba huu umetolewa kutuonyesha maana ya 'shetani'. Paulo alisema kuwa, kwa sababu ya mapendeleo yake ya kipekee katika ufunuo wa Mungu –

"Hayo nalipewa mwiba katika mwili, mjumbe wa Shetani ili anipige, nisije nikajivuna kupita kiasi" (2 Wakorintho 12: 7).

Hapa tena, maono ya othodoksi ya jadi yanaleta haja ya dhana kwamba Kristo alikuwa na shirika na alikuwa anatumia makusudi mabaya, adui mkubwa wa Mungu, kumwadhibu Paulo. Hii huduma ya ushirikiano wa Ibilisi ilikuwa kwa faida ya uzima wa milele kwa Paulo. Ndiyo maana tunawakilishwa hapa na Kristo na Ibilisi kwa ushirikiano wa pamoja kwa ajili ya mema ya Paulo!

Hayo ni matokeo ya maoni ya Ukristo wa jadi. Kwa yeyote ambaye ana dhana ya maandiko matakatifu ya uhusiano kati ya Kristo na Paulo, haya maoni potovu yanayomtambulisha Mungu wa maovu katika uhusiano wao haiwezekani. Lakini ni kwa busara na usawa kwamba Kristo, kwa upendo, aliweka juu ya Paulo mateso ya kimwili – yawe sehemu ya jumla, kwa sasa, tukiangalia athari ya dhambi duniani (kwa matumaini - Warumi 8:20) – ili apate kukumbushwa daima kuhusu udhaifu wa kimwili na utegemezi wake wa msaada kutoka kwa Mungu.

Ni kweli kuwa kwa mujibu wa nadharia ya jadi ya othodoksi. Mungu na 'Shetani' wanashirikiana, na Shetani kwa uaminifu anafanya matakwa ya Mungu kwa kuwatesa milele kwa milele wale wote ambao hawamfurahishi Mungu katika maisha haya mafupi. Lakini ingawa Shetani hapa anawakilishwa katika nadharia hii kama anayeshirikiana na Mungu, na hutumiwa na Mungu kuwatesa waovu, kwa wakati huo huo wanawakilishwa na picha tofauti ya vita vikali na ushindani kati yao, waking’ang’ania ‘roho isiyokufa 'ya kila mtu.

'KUTOLEWA KWA SHETANI'

Paulo alisema (l Timotheo 1:20) kwamba alikuwa amewatoa Humenayo na Aleksanda kwa Shetani, ili wafundishwe kutomtukana Mungu. Na vile vile, anawafundisha ndugu Wakorintho, kuhusu wahalifu kinyume na Ukweli waliokuwa katika Mwili –

"kumtolea Shetani mtu huyo, ili mwili uadhibiwe, ili na roho iokolewe katika siku ya Bwana wetu Yesu" (I Wakorintho 5: 5).

Maana ya 'kutolewa kwa Shetani' ni wazi kutoka kwa mazingira ...

"ili kwamba aondolewe miongoni mwenu huyo aliyetenda jambo hilo. (kifungu cha.2)

" MWONDOENI yule mbaya miongoni mwenu "(k. 13)

Na kusudi ya kusema ya kuondoa hayo kutoka kwa mwili -.

"Kwa uharibifu wa mwili, roho yake iweze kuokolewa katika siku ile ya Bwana" (k.5)

- ni vile vile ilivyoelezwa katika muktadha –

"Je, hamjui kwamba chachu kidogo huchachusha donge lote la unga? JISAFISHENI MKATOE ile chachu ya kale (viungo vyenu viovu) kwamba mpate kuwa donge jipya. "(k. 7)

'Roho ya kuokolewa Siku ile ya Bwana Yesu ni Roho na mwili safi, zilizosafishwa na kuhifadhiwa kwa kuondolewa kutoka humo kwa mambo ya dhambi, na ya kimwili ambayo, isipoondolewa, itatia 'chachu' na kuharibu donge zima. Kwa ulinzi bora wa mwili kutoka kwa chachu ya dhambi, na 'kutoa mtu kwa Shetani' ni kuwatoa nje katika ulimwengu wa Dhambi, ambapo wanatoka kama wenye dhambi, lakini kwa matumaini ya kuamshwa kwao na matengenezo mapya. Lakini kuwapa Ibilisi wa othodoksi ni kuwatupa katika ukosefu wa matumaini, kwa mateso ya kutokuwa na mwisho kuzimuni. Kama mtu angekua anatoa uamuzi wa hukumu ya mwisho ya mtu jambo la mwisho kufanya ingekuwa kumpa Ibilisi jitu wa kiothodoksi. Hiyo bila shaka sio madhumuni ya kutengwa na ushirika.

Amri nyingine wazi na halisi kuhusu 'kutolewa kwa Shetani' ni - "Mtu anayesababisha mafarakano baada ya kumwonya mara ya kwanza na mara ya pili, mkatae" (Tito 3:10).

"Jitengeni nafsi zenu na kila ndugu aendaye bila utaratibu… Kama mtu ambaye hatautii huu ujumbe wetu. . msishirikiane naye "(2 Wathesalonike 3: 6.14).

"Waangalieni wale wafanyao mambo ya kukwaza . . Jiepusheni na watu hao "(Warumi 16:17)

Lakini kusudi ni kurekebisha tabia, kwa matumaini, sio kumtupia hayawani au jitu la Ukristo wa jadi -.

"Msizungumze naye ili apate kuona aibu. Lakini msimhesabu kuwa adui, bali mwonyeni kama ndugu "(2 Wathesalonike 3:14 15)

Paulo anasema kwa waumini wa Thesalonike.

"Ningependa kuja kwenu, lakini Shetani alinizuia "(I Wathesalonike 2:18)

Tunapoangalia katika historia ya mfano huo, tunaona kwamba yale yaliyomzuia Paulo ilikuwa upinzani na mipango ya hila ya watu waovu, watu walioishi na kuendesha shughuli zao kwa mujibu wa mwenendo wa dhambi ya mwili. Kulikuwa na wengi ambao rekodi yao iko, lakini Ibilisi wa kiothodoksi.

'SHETANI' kATIKA KITABU CHA UFUNUO NI DHAHIRI KUWA INAZUNGUMZIA WATU

Wakati maana ya kijumla ya Ufunuo inaeleweka (na ni lazima ieleweke ili kupata kuelewa Injili kikamilifu), kumbukumbu katika Ufunuo 12 na Ufunuo 20 itaonekana kuwa yenye uadilifu dhidi ya nadharia ya Ibilisi jitu wa kiothodoksi; na kwamba chini ya istilahi 'Joka', 'Nyoka', 'Ibilisi' na 'Shetani': nguvu za kisiasa na nguvu dhidi ya dhambi ya mwili - (Warumi 8: 3) - inawakilishwa.

Hii nguvu ya Joka / nyoka / Ibilisi / Shetani ina vichwa 7 na pembe 10 (Ufunuo 12: 3), na tunaambiwa katika maelezo halisi juu ya ishara hizi (Ufunuo 17:12 14) kwamba pembe hizo 10 ni wafalme 10 ambao, katika wakati wa mwisho, watafanya vita dhidi ya Kristo wakati ambapo anarudi kuuweka chini ya miguu yake dunia na kuanzisha Ufalme wake. Wafalme hao wanahusiana (Ufunuo 17:18) na 'Jiji Kubwa ambalo lina mamlaka juu ya wafalme wa DUNIA. Hii ni picha ya kidunia kotekote.

Jiji kuu ambalo lilitawala dunia katika siku za Yohana, na kwa miaka mingi baadaye, na kwa karne zaidi mbeleni kwa njia mbalimbali (lakini halisi sana), lilikuwa ni Roma. Kwa hivyo Ufunuo imeweka nguvu ya Joka / Ibilisi / Shetani kama uingizaji wa kisiasa wa Dhambi ya mwili katika onyesho la utawala wake ulimwenguni.

NINI HUMSHAWISHI MTU KUTENDA DHAMBI? Mtazamo wa jadi ni kwamba kila mtu hujaribiwa wakati ananaswa na Shetani. Hii ni kweli - kama tunaelewa maana ya 'Shetani' Maandiko yanasema—

"Kila mmoja hujaribiwa na tamaa yake mwenyewe, huku akivutwa na kudanganywa. Halafu ile tamaa ikiisha kuchukua mimba huzaa dhambi." (Yakobo 1:14 15).

Itabainishwa kuwa 'Shetani' hatajwi popote katika mchakato huu. Huyu ni Shetani wa Biblia, kwa shughuli zake za kumjaribu na za kuvuta: 'tamaa ya mwili ";' sheria ya Dhambi katika viungo vyake.' Hebu tuwe na uhakika kuwa tunatambua na kupambana na adui halisi - DHAMBI - katika hali zake zote! Msingi na kina cha maarifa ya Mungu kupitia ujumbe ulio wazi wa maandiko utatuwezesha kufanya hivyo.

'KITI' CHA SHETANI PERGAMO

Kitambulisho cha Shetani, kwa upinzani uliopewa motisha na dhambi ya watu waovu kwa mambo ya Mungu unatolewa mfano zaidi katika Ufunuo 2:13, ambapo mtume Yohana anawasilisha ujumbe kutoka kwa Kristo kwa waumini waaminifu walioishi Pergamo –

"Najua unakoishi, hata pale ambapo kiti cha Shetani kilipo; nawe walishika sana jina langu ... hata katika siku zile za Antipa ambaye alikuwa shahidi wangu mwaminifu, aliyeuawa miongoni mwenu, mahali anapoishi Shetani."

Kwa mujibu wa dhana ya Ukristo wa jadi, 'kiti' cha Shetani - au makao makuu - kamwe hayakuwa Pergamo katika Asia Ndogo, lakini katika moto mkali unaowaka kuzimuni. Lakini Pergamo wakati huo ilikuwa kituo na ngome ya watu ambao wanaupinga Ukweli wa Mungu, na waliwatesa watu wake. Taswira hiyo iko wazi. Adui na Shetani mkubwa wa mtu ni akili yake ya kimwili, kuwili, kutoka ndani mwake, na mtu binafsi au upinzani uliopangwa na uhasama kutoka nje. Adui wa Ukweli wa watu wa Mungu ni Dhambi iliyojaza dunia kotekote, utawala wa kila aina duniani. Na hivi ndivyo Maandiko yanavyosawiri shetani.

SOMA WARUMI 7 KWA PICHA YA KWELI YA BIBLIA

Soma Warumi 7, ambapo inachambuliwa kwa undani zaidi. Hakuna kabisa kidokezo au mtajo wa kiumbe chochote kiovu, wala nafasi yoyote ya hoja ya kuzua mjadala kuhusu jitu hilo. Lakini tunapata kuona Dhambi ... kanuni za Dhambi katika mwili - kinagaubaga imehaiishwa kama adui mkubwa na chanzo cha maovu. Jaribu kumleta huyo mwenye kwato na pembe, Ibilisi wa ushirikina, taswira nzima itavurugika, kuchanganyikiwa na kukinzana. Yeye ni mwenzi anayekubaliwa wa Mungu, na wakati huo huo anatenda mambo ya ajabu mno na yenye mafanikio zaidi katika kutega 'roho zisizokufa’ kuliko Mungu.

Shetani jitu, hayawani wa uovu, anayetesa idadi kubwa ya watu milele na milele bila kikomo, hufanya mpango wa Mungu na kusudi lake na binadamu kuwa yenye hofu, ya kihayawani na yenye kushindwa kabisa; ya kutisha, kufisha, na kuzidisha mateso makubwa na maovu, kwa dunia milele na milele bila kikomo. Inaonekana vigumu kuamini kuwa hii ni hatima, kilele cha milele kwa madhumuni ya Mungu kwa wanadamu! Lakini nadharia ya kiasili na mafundisho ya kawaida ya Ibilisi jitu, nadharia ya kuzimu ya milele inaleta hazima hiyo.

Kwa bahati nzuri, Maandiko hayakubaliani na hayo. Kufikia hapa tumelenga hasa kueleza 'Ibilisi' na 'shetani' sivyo tunavyofikiria. Katika somo la tatu na la mwisho kuhusu suala hili muhimu tutachunguza kwa kina zaidi hasa Biblia inaonyesha shetani kuwa nani. Zoezi hili litaangazia baadhi ya vipengele muhimu sana vya Injili ambavyo ni muhimu katika kuelewa jinsi ubora wa Mungu umeonyeshwa na kutangazwa katika mchakato wa kuleta wokovu kwetu.

MASWALI kwa Somo la 19

1. Neno 'Shetani' linatokana na lugha gani?

2. Maana ya msingi ya neno 'Shetani' ni nini?

3. Je, watu binafsi wenye haki wamewahi kuitwa 'mashetani'? Toa mifano.

4. Maneno gani mengine yanaonekana katika AV (Toleo la Kiingereza/Kiswahili) yanayoashiria 'shetani'?

5. Watu waovu wamewahi kuwekwa katika kundi sawia na 'mashetani'? Toa mifano.

6. Kupitia kwa njia gani ndipo Watafsiri hawajakuwa waaminifu katika tafsiri ya neno 'shetani'?

7. Nani alikuwa 'Shetani' katika Zakaria 3?

8. Ni nani alileta maovu yote juu ya Ayubu? Toa maandiko katika kuthibitisha.

9. Ni kwa njia gani akawa adui wa Ayubu na uwezo wa kuleta mateso juu ya Ayubu?

10. Je, Mungu amewahi kuwa 'Shetani, au adui? Lini?

11. Kulikuwa na mtu yeyote mwenye haki katika Agano Jipya aliyewahi kuitwa 'shetani'?

12. Je, neno la Kiebrania 'shetani' ilitokeaje kutumika katika Agano Jipya, ambayo ni katika Kigiriki?

13. Ni nani aliyekuwa 'shetani' aliyemzuia Paulo kutembelea waumini Thesalonike?

14. Je, tunaweza kuwa 'mashetani' katika kupinga mapenzi ya Mungu, kama tunajaribu kwa dhati (kwa kutojua) kufanya yaliyo sawa? Toa mfano katika maandiko.

15. Inamaanisha nini 'kutolewa kwa Shetani, ili kujifunza wasimtukane Mungu'?

16. Je tunajuaje 'Shetani' wa Ufunuo ni ishara ya mashirika ya kibinadamu?

17. Ni nani aliyekuwa 'shetani' aliyewashawishi Anania na Safira katika Matendo 5?

18. Ni nini jaribio la nguvu zinazowashawishi watu katika maisha yao?

19. Ni nini chanzo cha maovu ya dunia yote?

20. Ni 'Shetani' yupi mkubwa ambaye lazima watu wote wamwogope na kumpinga na kumshinda?

21. Ni nguvu gani peke iliyo na uwezo wa kutusaidia kumshinda Adui huyu mkubwa?